



SWAHILI A1 – STANDARD LEVEL – PAPER 1
SOUAHLÉLI A1 – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 1
SUAHILI A1 – NIVEL MEDIO – PRUEBA 1

Monday 22 May 2006 (morning)

Lundi 22 mai 2006 (matin)

Lunes 22 de mayo de 2006 (mañana)

1 hour 30 minutes / 1 heure 30 minutes / 1 hora 30 minutos

INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Write a commentary on one passage only. It is not compulsory for you to respond directly to the guiding questions provided. However, you may use them if you wish.

INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N'ouvrez pas cette épreuve avant d'y être autorisé(e).
- Rédigez un commentaire sur un seul des passages. Le commentaire ne doit pas nécessairement répondre aux questions d'orientation fournies. Vous pouvez toutefois les utiliser si vous le désirez.

INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Escriba un comentario sobre un solo fragmento. No es obligatorio responder directamente a las preguntas que se ofrecen a modo de guía. Sin embargo, puede usarlas si lo desea.

Toa maoni yako juu ya moja ya tungo zifwatazo.

1. (a)

Twamshukuru Mwenyezi, kwawe mwingi ukarimu,
Alo na kiti cha enzi, Mola wetu Akramu,
Kutupa kitu azizi, lugha kuitakalamu,
Lugha ni kitu kitamu, ujuwapo kutumia.

- 5 Lugha mkuu mlezi, aleaye binadamu,
Hata wanyama ja mbuzi, wana lugha wafahamu,
Hufunguwa simulizi, izaayo tabasamu,
Lugha huwa ni imamu, ujuwapo kutumia.

- 10 Lugha hodari mkwezi, akweaye tata ngumu,
Huzifyeka pingamizi, zizushazo uhasimu,
Ikazindisha mapenzi, wapendanao kudumu,
Lugha huyeyusha sumu, ujuwapo kutumia.

- 15 Lugha ndiye mpagazi, mazito kuyahudumu,
Pia hupanga vizazi, pasi mbari kudhulumu,
Aidha hufanya kazi, ikawa mustakimu,
Lugha kwayo ni timamu, ujuwapo kutumia.

- 20 Lugha ni mpelelezi, waovu kuwakasimu,
Huwatoa palo wazi, kushuhudia kaumu,
Yasifiwa na wajuzi, kuwa ni kito adhimu,
Lugha mkuu hakimu, ujuwapo kutumia.

Lugha huizuwa kazi, katakaza mahakimu,
Huwaacha kanwa wazi, wakili kitakalamu,
Muhalifu na jambazi, wakaishinda hukumu,
Urongo huwa timamu, ujuwapo kutumia.

- 25 Lugha iwe ni kingozi, kizungu au kiamu,
Iwekapo wazi wazi, silabi na tarakimu,
Huyakimu maongezi, yakasikizwa kwa hamu,
Lugha huwa ni muhimu ujuwapo kutumia.

30 Lugha ni mpambanuzi, wanyonge na wajukumu,
 Kadhalika ni jahazi, ya nohodha muhitimu,
 Kufamaji haiwezi, si vina si milizamu,
 Lugha maji zam-zamu, ujuwapo kutumia.

Kutoka: *Malenga wa Vumba*, Bougheit Amana 1982.

- Fafanua dhamira na maudhui ya shairi hili.
- Mwandishi ametumia mtindo gani ili kuitisha ujumbe wake.
- Kulingana na mshairi lugha ina umuhimu gani katika jamii?

1. (b)

Majitu daima vilikuwa viumbe vilivyonitisha katika jumla ya hadithi nyingi alizotutambia nyanyangu. Aghalabu yalimkabili mtu akiwa pekee, bila ya tumaini wala kimbilio lolote la kuijiope na makucha yake marefu na meno yake makubwa yenyenye makali ya msumeno. Jitu lilikuwa nabii wa aina yake. Kama sivyo, liliujuje wakati wa kuyashambulia na kuyahujumu 5 mawindo yake? Hufika pale ambapo binadamu yuko dhalili. Halafu likishafika, hupanua mdomo wake au midomo katika sehemu nyingi za miili yao. Sehemu kama kisogo, mgongo na hata kwenye mapaja zilikuwa na midomo.

Jana usiku nilikuwa natafakari kuhusu viumbe hawa wa ajabu. "Watu waliwezaje 10 kuwaani na kuwapuliza uhai?" Nilijiuliza kimoyomoyo. "Pengine waliishi." Nilijaribu kujiamulia bila uhakika. "Huenda walikuwepo na kukaribiana na akina sisi, nyanya zetu na baba zetu," ilinijia tena.

Nimesikia kwamba hapo zamani za kale, palikuwepo viumbe vilivyomzidi nguvu mwanadamu mara elfu. Sijui kama hayo ndiyo Majitu tunayotambiwa hadithi juu yake. Hapana ithibati za 15 kutegemewa kuhakikisha dai hili. Lakini kila nilifikiriapo kuhusu hadithi za bibi, mambo mengi hujichora mbele ya macho yangu. Wakati mwagine, akili yangu huchora picha za kutisha na kunipa hisia ndivyo yalivyokuwa majitu.

Kuna huyu mhunzi maarufu aliyehamia ughaibuni kwenda kusana. Huku amemwacha mkewe 20 mjamzito peke yake. Punde tu alipoondoka, jitu moja kali lilitokea kwa ghafla. Likabweka kwa furaha na kujivunia uwezo wake. Kisha, likamuuliza maswali ya kijinga na kikatili. Hatimaye, likamtesa na kumfanyiza kazi zingine za shokoa.

Kutoka: *pendo la Heba* (Wahariri) K. Kingenia na M. Wafula (1996)

- Chambua kwa mapana na marefu maudhui muhumu katika makala haya.
- Mwandishi ametumia mtindo gani ili kuitisha ujumbe wake?
- Onyesha kwa ukamilifu vile mwandishi anavyoelezea sifa na maumbile ya majitu kulingana na makala haya.